## 1. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kunilinda na kunipa nguvu na maarifa zaidi ya kusonga mbele na kuendelea kuwatumikia wananchi wangu wa Jimbo la Momba. Aidha, napenda kumshukuru KUB Mhe. Freeman A. Mbowe (Mb) kwa kuniteua kuwa Naibu Msemaji Mkuu wa wizara hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, pia natoa ahadi kwake nakwa chama changu CHADEMA, na wananchi wote wapenda mageuzi kwamba, nitaitumikia nafasi hii kwa uadilifu mkubwa na kwa moyo wangu wote.

**Mheshimiwa Spika,** hali kadhalika nitumie fursa hii kwa namna ya pekee kumshukuru Mheshimiwa Halima James Mdee (Mb) Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii kwa kazi kubwa tulioifanya ya kuandaa hotuba hii, pia nitoe pongezi na kuwatia moyo Makamanda wote waliotolewa Bungeni kwa hila, ninasema mapambano yanaendelea na tuko pamoja.Aidha niwashukuru waheshimiwa wabunge wote wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa ushirikiano na umoja wetu.

## 2. WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO-Fungu 50

**Mheshimiwa Spika,**Wizara ya fedha na Mipango ndio yenye mamlaka makubwa zaidi katika uchumi wa Tanzania. Wizara hii;

i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla

ii) Kusimamia ukusanyaji wa mapato ya ndani na nje ya nchi pamoja na matumizi yake (kwa mantiki hiyo wizara ambazo hazikupata fedha kwa kadiri zilivyopitishwa na Bunge,maelezo yake ni kuwa hazikupata fedha hizo kutoka wizara ya fedha )

iii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali

iv) Kufuatilia utekelezaji wa mipango ya kupunguza umasikini katika sekta mbali mbali

v) Kusimamia deni la Taifa

vi) Kusimamia upatikanaji wa rasilimali fedha zinazopatikana katika miradi ya ubia baina ya serikali na sekta binafsi

vii) Kusimamia sera, sheria ,kanuni na taratibu za uhasibu, ukaguzi wa ndani na ununuzi wa Umma,

viii) Kusimamia Mali za serikali,taasisi na mashirika ya Umma (treasurer registrer)

ix) Kusimamia masuala ya Tume ya Pamoja ya fedha

x) Kuandaa na kulipa mishahara watumishi serikalini

xi) Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni ya wastaafu nakudhibiti biashara ya fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi. Hivyo bajeti ya wizara hii inatakiwa kutekeleza majukumu haya ya wizara.

**Mheshimiwa Spika,** kwa majukumu hayo ya wizara, ni dhahiri kwamba uendeshaji wa nchi hii uko chini ya wizara hii ya fedha, hivyo kuporomoka au kupanda kwa uchumi ni jukumu la wizara ya fedha. Ile ***"kauli mbiu ya Serikali"*** ya kuwa na uchumi wa viwanda wakati inaelewa kabisa kuwa jambo hilo kwa miaka ya hivi karibuni haiwezekani kabisa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imetumia neno kauli mbiu kwa ukweli kwamba mpango huo hauna tofauti na zile kauli mbiu za siasa ni kilimo, kilimo ni uti wa mgongo n.k na mwisho kauli mbiu hizo zilishindwa kutekelezeka na kuzaa matunda kutokana na kukosekana kwa uwekezaji kwa mipango hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** jambo hilo la uchumi wa viwanda ni sawa kabisa na pale baba mwenye nyuma kuwa na mboga na kutegemea kupata ugali au wali kutoka kwa jirani. Na tukumbuke kwamba kila mkataba wa fedha

kwa kila mradi wa aina yoyote utakaotekelezwa hapa nchini ni lazima upitie na kuidhinishwa na hazina.

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya fedha inaelewa vizuri kwamba kutokana na hali halisi ya Tanzania na upatikanaji wa fedha za ndani na za nje itakuwa ni vigumu kwa nchi yetu kutoa elimu bora na ya bure. Kwani, ukweli ni kwamba kizuri ni gharama na hivyo hutoaji wa elimu iliyo bora ni lazima kufanya uwekezaji mkubwa na sio kubabaisha na mwisho kuishia njiani bila ya kutimiza lengo.

**Mheshimiwa Spika,** ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii, kuhakikisha inatoa ushauri sahihi kwa Mheshimiwa Rais, badala ya ushauri usio na tija kwa taifa kama suala la sukari nchini na namna ya utekelezaji wa kutoa elimu bure. Mambo ambayo mpaka sasa yanaonekana kuishinda serikali ya awamu ya tano.

## 2.1. JUKUMU LA KUSIMAMIA UTEKELEZAJI WA BAJETI 2015/16

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ina jukumu la msingi la kupanga bajeti, na kusimamia utekelezaji wake. Ili kupima ufanisi wa Wizara hii ni lazima kufanya uchambuzi wa nini kilipangwa?nini kilipatikana na utekelezaji wake. Uchambuzi huu utatupa dira ya kujua uwezo wetu wa

makusanyo na hatimaye kuwa na bajeti zinazotekelezeka!

**Mheshimiwa Spika,**wizara ya fedha imekuwa na jukumu la kupeleka fedha zote zilizopangwa kwenye bajeti kwa kila wizara lakini mpaka sasa utekelezaji wake ni hafifu na inaonyesha wizara kushindwa kabisa kusimamia jukumu hili. Mifano ya wizara ambazo wizara ya fedha na mipango imeshindwa kupeleka fedha ni pamoja na;-

**Wizara ya mambo ya ndani**, Kati ya fedha zote zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya Wizara, mishahara ilikuwa 52%, matumizi mengineyo ilikuwa 47% na kwa upande wa bajeti ya maendeleo ni 1% tu.[1]

**Wizara ya afya**: bajeti ya maendeleo iliyotengwa 2015/16, hadi robo ya tatu ya mwaka hakuna fungu hata moja ambalo wizara hiyo ilikuwa imepata zilizoidhinishwa na Bunge kwa angalau 50%,halikadhalika Fungu 52 – Idara kuu Afya hadi kufikia tarehe 31 March 2016 kiasi cha fedha kilichopokelewa ni 31% tu ya Bajeti, **Wizara ya kilimo** katika kipindi cha mwaka 2015/16, hadi mwezi March, fedha za maendeleo zilizokuwa zimepatikana ni bilioni 5.1 ambazo ni sawa na 15.9% ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge.

[1] Taafira ya Kamati ya Bunge ya mambo ya nje , ulinzi n usalama, 2016/17, pg. 8

**Mheshimiwa Spika,** hii ni mifano michache tu, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema Wizara ya Fedha inawafanyia watanzania mchezo wa kuigiza kwa kutayarisha kile kinachoitwa **"nominal budget"** badala ya kutayarisha **"real budget".** Kwa mazingira hayo ya upatikanaji wa fedha za maendeleo ambapo utekelezaji wa bajeti za maendeleo unakuwa chini ya asilimia 50, inawezekanaje serikali kufikia **uchumi wa viwanda** chini ya usimamizi wa wizara hii ambayo imekuwa ikishindwa kutekeleza majukumu yake ya kutoa fedha kama zilivyopangwa?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inarudia tena kuwa wizara hii inajukumu kubwa hivyo inatakiwa itekeleze majukumu yake kwa uadilifu na uhakika, kinyume cha hapo mipango yote itakuwa ni ngonjera tu na miaka inazidi kupita na Tanzania badala ya kwenda mbele inarudi nyuma.

## 3. KITENGO CHA KUDHIBITI UTAKATISHAJI WA FEDHA HARAMU- (FIU) -Fungu 13

**Mheshimiwa Spika,**Benki Kuu ya Tanzania ni benki ya kitaifa inayosimamia masuala ya kibenki na kifedha. Kati ya majukumu yake ni utoaji wa fedha za Tanzania, Shilingi yaTanzania. Benki Kuu ya Tanzania iliundwa na Sheria ya Benki ya Tanzania 1965. Mwaka 1995, baada ya

kuonekana kuwa benki hii ina majukumu mengi kuzidi uwezo wake,Sheria ya Benki ya Tanzania 1995 ilipitishwa na kuipa benki hii jukumu moja ambalo ni kusimamia sera ya fedha nchini.

### 3.1. Udhaifu wa Muundo wa Financial Intelligence Unit (FIU)

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatilia mashaka uwezo na dhamira ya Benki Kuu kufanya ujasusi wa Miamala ya fedha katika kuzuia utakatishaji wa fedha sambamba na uwezo mdogo wa Kitengo cha Financial Intelligence Unit, kitengo ambacho kinazuia utakatishaji wa fedha haramu.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeunda kitengo cha Financial Intelligence Unit (FIU) ambacho kina mamlaka ya kiutawala pekee na huishia kufanya uchambuzi wa taarifa za miamala ya fedha na kuziwasilisha ama Jeshi la Polisi au PCCB, wakati huo huo PCCB inalazimika kupitia kwa Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP) ili atoe ruhusa ya kufungua mashitaka.

**Mheshimiwa Spika,** matokeo yake ni kuwa FIU haina uwezo wa kufanya uchunguzi, wala kuendesha mashitaka dhidi ya utakatishaji wa fedha haramu jambo ambalo ni mwanya unaotumiwa na watu waovu na

mafisadi kama ilivyokuwa katika wizi wa Mabilioni ya Rada, wizi wa fedha kwenye akaunti ya Tegeta Escrow na wizi wa fedha katika Mkopo wa Serikali dola milioni 600 kutoka Stanbic Bank.

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa FIU ya Tanzania ni "administrative model" wakati mfumo imara zaidi ni ule wa "Judicial Model" ambao unakiongezea nguvu kitengo hicho cha kuzuia miamala ya biashara haramu za kutakatisha fedha.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa "Egmont[2] Group of Financial Intelligence Units" Judicial Model of FIU inamaanisha kuwa

*"The Judicial Model is established within the judicial branch of government wherein "disclosures" of suspicious financial activity are received by the investigative agencies of a country from its financial sector such that the judiciary powers can be brought into play e.g. seizing funds, freezing accounts, conducting interrogations, detaining people, conducting searches, etc."*

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Ungeni inaishauri Serikali kuimarisha kitengo cha FIU kwa kukiundia Mfumo wa Judicial Model ili kuepuka aibu ambayo Taifa letu imekuwa ikiipata kutokana na

[2] http://www.egmontgroup.org/about/financial-intelligence-units-fius retrieved at Egmont Group on 28.05.2016, Financial Intelligence Units

***Serious Fraud Office*** ya Uingereza kuwana na uwezo wa kurudisha fedha za zilizoibiwa kwa njia ya kifisadi wakati kazi kama hiyo ingeweza kufanywa na vyombo vya hapa nchini endapo vingeimarishwa kama ambavyo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inavyoshauri kuimarisha kitengo cha FIU.

## 4. OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI- Fungu 45

### 4.1 Kupunguzwa kwa Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilianzishwa chini ya Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, na kufafanuliwa na sharia ya Ukaguzi ya umma, Na.11 ya mwaka 2008(kama ilivyorejewa) na kufafanuliwa na kanuni za Ukaguzi wa umma za mwaka 2009.

**Mheshimiwa Spika,** Lengo kuu la Ofisi hii ni kutoa huduma bora za ukaguzi zenye kuleta tija kwa nia ya kuimarisha uwajibikaji unaozingatia thamani ya fedha katika kukusanya na kutumia rasilimali za umma.

**Mheshimiwa Spika**, ili ofisi hii iweze kutimiza malengo yake kwa ubora, uadilifu na ubunifu wa hali ya juu inahitaji rasilimali fedha za kutekeleza hayo yote. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

ilikuwa imeomba Shilingi **69.839 Bilioni** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **8.0 Bilioni** kwa matumizi ya maendeleo, lakini Kiasi hicho kilipunguzwa na Serikali hadi na kuiwekea ukomo wa Shilingi **28.3 Bilioni** kwa matumizi ya kawaida na Shilingi 4.0 Bilioni, matumizi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** ni ukweli usio nashaka kwamba Ofisi hii kwa kiwango kikubwa imesaidia kuokoa mabilioni ya fedha ambazo zilikuwa zinatumiwa nje ya malengo na pia kugundua wizi na ukwepaji wa kodi ambao ulikuwa ni **donda ndugu** katika utumishi wa umma au kwa maneno mengine walivunja mtandao wa wizi uliokuwa unaelekea kuota mizizi kati ya watendaji Serikali na wafanyabiashara wasio waaminifu. Hivyo basi kitendo chochote cha kupunguza bajeti yao ya kufanyia kazi maana yake ni kuwafanya watendaji wasiwe na uwezo wa kutenda kazi zao kwa kiwango kilichowekwa na ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** CAG amekiri kuwa "Hatua ya kushusha ukomo wa bajeti ya Fungu 45 itasababisha kupungua kwa uwezo wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kutekeleza jukumu lake la kukagua na kudhibiti matumizi ya rasilimali za umma" Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaiona hatua hii kuwa ni dhamira ya Serikali ya CCM ya awamu ya tano kukwepa kuwajibishwa na kuua kabisa

dhima nzima ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kama taasisi ya kusimamia uwajibikaji wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** CAG amekiri kuwa ukomo wa bajeti uliowekwa na Serikali utaathiri kabisa ukaguzi wa hesabu za Serikali katika maeneo 9, ambayo ni;

(i) Ukaguzi wa Serikali Kuu
(ii) Ukaguzi wa Hazina ikiwemo Mamlaka ya Mapato Tanzania na Deni la Taifa
(iii) Ukaguzi wa Serikali za Mitaa ambapo fedha nyingi zinaelekezwa katika ngazi za kata na vijiji
(iv) Ukaguzi wa Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali
(v) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo inayofadhiliwa na Washirika wa Maendeleo
(vi) Ukaguzi wa Ofisi za Balozi za Tanzania nje ya nchi;
(vii) Maboresho katika Ukaguzi;
(viii) Ujengaji uwezo wa Wakaguzi; na
(ix) Uendeshaji wa Ofisi za Ukaguzi zilizopo Katika Mikoa yote ya Tanzania Bara.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaliomba bunge lako tukufu na wabunge wote kwa ujumla bila kujali itikadi zetu za siasa, kupitia Kamati ya

Bunge ya Bajeti kupitisha azimio la kuongeza ukomo wa fedha za fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kufikia Shilingi **69.839 Bilioni** kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti ya mwaka 2015, kifungu cha 8 (e) kinacholipa bunge mamlaka ya kuishauri Serikali kuhusiana na vifungu vya bajeti.

**Aidha, Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaliomba Bunge kuangalia uwezekano wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, vitabu vyake vya hesabu na maombi ya fedha kufanyiwa kazi na kamati ya kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), badala ya ilivyo sasa ambapo inasimamiwa na Kamati ya Bajeti.

## 5. DENI LA TAIFA-Fungu 22

**Mheshimiwa Spika,**Wizara ya fedha ya fedha ina jukumu pia la kusimamia deni la Taifa,Deni la Taifa limeendelea kuwa changamoto kubwa sana kwa uchumi wetu. Hakuna ubishi kwamba kukua kwa deni la Taifa kunaisababishia serikali kuendelea kuwa tegemezi na hivyo kushindwa kutatua kero za kiuchumi za wananchi. Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha serikali imeendelea kukopa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara hali ambayo inazidi kufanya hali ya maisha kwa wananchi iendelee kuwa ngumu kwa kuwa serikali inatumia fedha nyingi kulipa madeni **badala ya**

**kuzitumia fedha hizo kugharamia miradi ya maendeleo.Tutarajie deni hili kuongezeka kwa kiwango kikubwa sana kwa kuwa kwa mwaka huu pekee tunatarajia kukopa mkopo wa biashara(wa ndani na nje) wenye thamani ya shilingi trillion 7.4**

**Mheshimiwa Spika**,Kitabu cha Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2016/17, kilichotolewa na wizara ya fedha na Mipango, **April 2016**, kinaeleza kwamba hadi kufikia **Januari 2016, deni la taifa limefikia dola za kimarekani 19.521**(sawa na shilingi trillion 42.9) na kwa nyongeza ya shilingi shilingi trillion 7.4 kwa mwaka ujao wa fedha (2017/18) deni la taifa litafikia trillion kati ya trillon 48- 50! Ikumbukwe ni mwaka 2008 (miaka 8 tu iliyopita) deni la Taifa lilikuwa shilingi Trillion 7.8!!kasi ya ukopaji wa mikopo mikubwa yenye masharti ya kibiashara ina athari kubwa kwenye uhimilivu wa deni.

**Mheshimiwa Spika,**Licha ya kwamba Serikali ya CCM inajinasibu kuwa inakopa fedha hizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo ,takwimu za utekelezaji wa mpango wa Taifa wa miaka 5 tulizoziainisha hapo juu, zinadhihirisha kwamba mikopo hii haijasaidia kubadilisha hali ya maisha ya wananchi!Na mbaya Zaidi wananchi hawa hawa ndio wanawajibika kulipa deni kwa njia mbali mbali ikiwemo kodi!

**Mheshimiwa Spika**, ikumbukwe kwamba deni hili halijajumuisha madeni ya mifuko ya hifadhi ya jamii, mikopo ya halmashauri na madeni mbalimbali ambayo yameingizwa kimakosa ofisi ya msajili wa hazina.

## 5.1. ATHARI ZA DENI LA TAIFA KATIKAUTEKELEZAJI BAJETI

**Mheshimiwa Spika,Mwenendo wa matumizi unaonyesha kwamba,** Hadi kufikia Machi 2016 serikali imetoa mgao wa matumizi (Exchequer issues) wenye thamani ya shilingi bilioni 15,271 kwenda kwenye mafungu mbali mbali kwa ajili ya utekelezaji wa bajeti. **Kati ya kiasi kilichotolewa shilingi bilioni 12,247 zilikuwa ni za matumizi ya kawaida** na ikijumuishha shilingi **bilioni 4,744.6 kwa ajili ya mishahara** na shilingi bilioni 2,350.1 kwa ajili ya matumizi mengineyo (ambapo matumizi ya Halmashauri yanayotokana na mapato ya ndani shilingi bilioni 117.7) . **Shilingi bilioni 5,035 zilitolewa kwa ajili ya kugharamia Mfuko Mkuu wa serikali**.

Mchanganuo wa shilingi bilioni 5,035 za mfuko mkuu wa hazina:

i) Malipo ya riba kwa madeni ya ndani na nje – bilioni 992.3

ii) Matumizi ‘mengine’ ya mfuko Mkuu (CFS others) – bilioni 760.7 (nimatumizi gani ya kiasi hicho cha fedha?)

iii) Malipo ya Mkopo ( Principal payment)-bilioni 3,282.3

iv) Malipo ya mkopo wa nje – bilioni 448.3

v) Malipo ya dhamana na amana za serikali zilizoiva bilioni 2,834.0

**Mheshimiwa Spika,** Katika bajeti yote ya 2015/16 ya shilingi bilioni 22,495, fedha iliyotolewa Kwa ajili ya matumizi yamaendeleo nishilingi bilioni 3,023 tu! Ambapo shilingi bilioni 2,645 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 378.9 ni fedha za nje. Wakati huo fedha iliyotumika kulipa deni ni shilingi bilioni 7,552( trillion 7.5)[3]

### 5.2. UHIMILIVU WA DENI LA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,**Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa muda mrefu imekuwa ikiitaka serikali ipunguze au iachane kabisa na mikopo yenye masharti ya kibiashara ambayo inazidi kuliongeza deni la Taifa. Hata hivyo serikali ya CCM imeendelea kupuuza mawazo haya mazuri kwa kisingizio kwamba deni husika ni himilivu. Na

[3] Maelezo ya waziri wa fedha na Mipango kwenye Kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa Bajeti yam waka 2015/16 kwa kipindi cha Julai 2015 hadi Machi ,2016 na mwelekeo hadi Juni ,2016. Mei 2016 uk. 9 na 10.

kwamba nchi yetu inakidhi vigezo vya kimataifa vya kukopesheka!

**Mheshimiwa Spika,**Ripoti ya Tathmini ya kina ya Mpango wa Taifa wa miaka 5[4] inaeleza kwamba japokuwa thamani ya sasa ya deni kwa pato la Taifa ni 24.83% ,ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 50%. Ripoti husika inatoa tahadhari kwamba kiwango hiki kimekuwa kikiongezeka kwa kasi toka mwaka 2010. (2011 - 14.9% ya pato la Taifa, 2012- 18% ya Pato la Taifa na 2013- 24.83% ya Pato la Taifa).**Na kwamba ongezeko hili ni kiashiria cha uwezo mdogo wa kiuchumi kulipa deni .** Inasikitisha sana pale ambapo kuna kuwa na upotoshaji kwa upande wa serikali pale tunapohoji kuhusiana na deni la Taifa na uhimilivu wake.

**Mheshimiwa Spika,** Ikumbukwe madeni tunayoyazungumzia hapo juu hayajajumuisha madeni yanayotokana na 'Malimbikizo ya Madai' ambayo watoa huduma mbalimbali wanaidai serikali. Hadi kufikia desemba 2015 Serikali ilikuwa imepokea madai mbalimbali yenye jumla ya shilingi bilioni 2.753. Kati ya hizo watoa huduma na bidhaa (goods and services) shilingi bilioni 1,182/-, madai ya umeme,maji na simu shilingi bilioni 137.2, madai ya pango la ofisi shilingi bilioni

[4] The United Republic of Tanzania, Comprehensive Review Report for Tanzania Five Year Development Plan 2011/2012-2015/16

53.4, wakandarasi mbalimbali (Construction work) shilingi bil.1,247 na madai ya watumishi yasiyo ya kimsharara sh bn 133…[5]''

**Mheshimiwa Spika,**Kambi rasmi ya upinzani inarudia tena hoja yake iliyotolewa kwa kipindi cha miaka mitano iliyopita, ili kujiridhisha kwamba deni la Taifa ni **'HIMILIVU'kama**inavyodaiwa:

Tunaitaka ofisi ya mthibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za serikali afanye ukaguzi maalum (Special Audit) katika kitengo cha deni la Taifa (Fungu 22) ili tuweze kujua mikopo tunayoichukua kila mwaka inatumika kufanyia nini, atoe taarifa ya miradi iliyotekelezwa kutokana na mikopo hiyo kama ni ya miradi ya kipaumbele kwa mujibu wa mpango wa Taifa wa Maendeleo. Halikadhalika ukaguzi huu maalum utatuwezesha kama Taifa kujua kiwango halisi cha deni la Taifa ambalo tunadaiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali itenganishe deni halisi la Taifa na matumizi mengineyo yanayohusu Mfuko Mkuu wa Hazina ili kuziba mianya ya ubadhirifu au matumizi mabaya ya fedha za umma kwa kisingizio cha Deni la Taifa.

[5] Maelezo ya waziri wa fedha na Mipango Mhe. Dk. Philip I Mpango (MB) kwenye kamati ya kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu tathmini ya hali ya uchumi na mwenendo wa utekelezaji wa Bajeti ya 2015/16 kwa kipindi cha julai hadi Desemba 2015 na mwelekeo hadi juni 2016, Machi 2016

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka 2015 deni la taifa lilikuwa ni shilingi bilioni 33,539.8 na Pato halisi la taifa kwa kipindi hicho lilikuwa ni shilingi trilioni 44.1. Kwa mujibu wa mahesabu ya uhimilivu wa deni kwamba Deni la Taifa kwa Pato la Taifa ili liwe na uhimilivu ukomo wake uwe asilimia 50.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mahesabu hayo inaonekana kuwa asilimia ya uhimilivu kwa sasa ni asilimia 76. Kwa kuweka Kumbukumbu sahihi wakati wa Mheshimiwa Saada Mkuya Salum (Mb) akiwa Naibu Waziri wa Fedha alisema ukomo wa uhimilivu wa deni ni 50%. Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufafanuzi wa uhimilivu wa deni letu.

## 6. OFISI YA MSAJILI WA HAZINA –Fungu 7

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Msajili wa Hazina iliyo chini ya wizara ya fedha ina jukumu la kusimamia uwekezaji na maslahi ya serikali katika mashirika ya umma na taasisi nyingine.[6] Ofisi hii imepewa jukumu la kudumu la kusimamia uendeshaji wa biashara na mambo ya watumishi wa bodi ambapo msajili wa hazina ana maslahi nako ama anamiliki.Ofisi hii inasimamia mashirika/taasisi za umma zipatazo 216. Serikali ina umiliki

[6] Ilianzishwa kwa Sheria ya Msajili wa Hazina (Mamlaka na Majukumu) Sura 370 ya mwaka 2002 na marekebisho yake mwaka 2010

wenye thamani ya shilingi bilioni 22,678.16 hadi tarehe 30 Juni 2015.

### 6.1. USIMAMIZI USIORIDHISHA WAUWEKEZAJI NA MASLAHI MENGINE YA TAIFA

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa serikali imebainisha kwamba wakati wa ukaguzi amebaini Kupungua kwa uwekezajiwa serikali katika mashirika na taasisi nyingine na wakati mwingine kupungua kwa hisa zake ,kutokana na serikali kushindwa kuongeza mtaji wakati ulipohitajika kwenye mashirika na taasisi ilizowekeza kupitia fursa ya haki ya kununua hisa za ziada na mpya. Hali hii husababisha nguvu ya serikali katika kufanya maamuzi kupungua , na hatimaye kupungua kwa uwezo wa serikali kupata gawio.Licha ya umuhimu wa ofisi hii, katika mwaka wa fedha 2015/16 ofisi ya msajili wa hazina ilitengewa shilingi **169,017,000,000 (Bilioni 169)** kwa ajili ya kulipia madeni na kurekebisha mashirika yenye matatizo ya mitaji. Serikali ya CCM iliishia kutoa shilingi **bilioni 10** tu! Ni uwendawazimu kupongeza mgao wa fedha, pasipo kuangalia kiasi kilichotolewa!

**Mheshimiwa Spika,**Kumekuwa na udhaifu mkubwa sana wa ushiriki wa Ofisi ya Msajili wa Hazina katika Mikutano Mikuu wa mwaka katika taasisi ambazo kuna uwekezaji wa serikali,hii inatokana na msajili wa hazina kutegemea

ruzuku kutoka serikalini ambayo haikidhi mahitaji ya kuweza kusimamia mashirika ya umma na binafsi ambayo serikali ina hisa.Ofisi ya msajili wa Hazina hukusanya gawio, mapato mengineyo na michango kutoka katika makampuni wanayoyasimamia.Fedha zote zinazokusanywa na msajili wa hazina hupelekwa serikalini kwa sababu Msajili wa hazina hayupo kwenye mpango wa bakizo (retention scheme). Hivyo uwezo wa msajili kuhudumia au kusimamia mashirika yaliyochini yake ni duni sana.

**Mheshimiwa Spika,** Katika taarifa ya Msajili wa hazina ya 30th June 2012 shirika hili halikuwemo katika listi ya Mashirika ya Umma. Na hakuna uthibitisho wowote wa uhalali wa kuondolewa. Utapeli huo huo umetokea kwenye shirika la UDA(ambao sasa hivi wanakumbatiwa na serikali ya CCM katika uendeshaji wa mabasi ya mwendo kasi).[7]UKAWA ambao tumepewa jukumu la kuongoza jiji la Dar es salaam, tutapambana usiku na mchana kuhakikisha udhalimu huu wa uporaji wa shirika la wakazi wa jiji la Dar es salaam haufanikiwa. Ni Imani yetu nia hii njema ya UKAWA itaungwa mkono na Mhe. John Pombe Magufuli.

[7] The United Republic of Tanzania, National Audit Office, Annual General Report of the controller and auditor General, on the Audit of Public Authorities and other Bodies for the financial Year 2014/15, pg 12-16

### 6.2 MASHIRIKA /MAKAMPUNI YASIYOTOA GAWIO SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika,**Wakati serikali ikilalama juu ya ukosefu wa fedha, taarifa ya Msajili wa hazina [8] inabainisha kwamba kuna kampuni ambazo serikali ina ubia lakini haitoi gawio.HususanKampuni za kibiashara ambazo serikali ina hisa chini ya 50%. Kuna Kampuni 33 (kama zilivyoainishwa hapa chini) ambazo ambazo serikali ina hisa na Licha ya kwamba yanatakiwa kutoa gawio serikalini, Ni kampuni 'chache' ambazo zinatoa gawio kutokana na faida zinazopatikana.

| KAMPUNI | HISA |
|---|---|
| 1. Abood seed Oil Industries Limited / abood soap | 20% |
| 2. Airtel Tanzania | 40% |
| 3. Aluminium Africa Ltd (ALAF) | 24% |
| 4. Datel Tanzania Limited | 35% |
| 5. East African Cables (Tanzania) Ltd | 29% |
| 6. Friendship Textile Co. | 49% |
| 7. Industrial Promotion services (Tanzania) ltd | 18.16% |
| 8. Inflight Catering services co/LGS Skychef | 20% |
| 9. Kariakoo Market Corporation | 49% |
| 10. Keko Pharmaceuticals Industries (1997) Ltd. | 40% |
| 11. KilomberosugarCo. | 25% |
| 12. MbeyaCementCo.Ltd | 25% |

[8] Ibid

13. Mbinga CoffeeCuring 43%
14. MboziCoffeeCuring 32%
15. MoshiLeather 25%
16. Mwananchi Engineering and Construction Co. 25%
17. National Bank of Commerce (NBC) 30%
18. National Microfinance Bank (NMB) 30%
19. New Africa Hotel 23%
20. Tanelec Limited 30%
21. Tanganyika Planting Co. (TPC) 25%
22. TANICA 7.67%
23. TANSCAN TIMBER CO. LTD 49%
24. Tanzania Breweries Ltd 4%
25. Tanzania Cigarette co. ltd 2.5%
26. Tanzania development Finance Ltd 32.1%
27. Tanzania Nationa Re-Insurance Corporation 1 Golden share
28. Tanzania Oxygen ltd 9.59%
29. Tanzania Pharmaceutical Ltd 40%
30. Tanzania Pipeline Ltd 33%
31. TLL Printing &Packaging Limited 25%
32. Usafiri Dar es salaam 49%
33. Williamson Diamond Limited 25%

**Mheshimiwa Spika**,Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni,inaitaka serikali ilieleze Bunge hili tukufu , kati ya kampuni tajwa hapo juu, ambazo zinatuhumiwa na Msajili wa hazina kutokutoa gawio(kwa lugha nyingine yanawaibia watanzania),zipi zinazotoa gawio serikalini,

na zinatoa kiasi gani? Na zipi hazitoi gawio na kwa sababu gani?

### 6.3. UWEKEZAJI WA TAASISI/MASHIRIKA YA UMMA USIO NA TIJA

**Mheshimiwa Spika,**Taasisi/ Mashirika mengi ya serikali yameingia katika uwekezaji wa majengo na makazi ya kibiashara ambao unatumia fedha nyingi na unachukua kipindi kirefu na mapato yanayotokana na uwekezaji kuwa kiduchu hivyo kusababisha taasisi hizo kutokupata faida inayostahiki.Na mbaya zaidi Taasisi nyingi zimekuwa zikiwekeza katika eneo moja na kumlenga mteja mmoja hivyo kusababisha majengo mengi kukosa wapangaji. Taasisi za mifuko ya hifadhi ya jamiii ya PPF, PSPF, NSSF , LAPF na GEPF zimekuwa zikitumia michango ya wanachama wao katika uwekezaji huo , hali hii inahatarisha usalama wa fedha za wanachama pichi zinapohitajika na wahusika .

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa NSSF pekee, kwa uchache tu umewekeza fedha za wanachama zipatazo shilingi trilion1.381.Fedha hizi ni mbali na fedha ambazo wameikopesha Serikali kujenga majengo mbalimbali kama vile Mchinga Complex, Chuo kikuu cha Udom,ujenziwa daraja la Kigamboni n.k.

Mifano michache ya miradiya nyumba za NSSF;

i. Nyumba 300 za Mtoni Kijichi (PHASE I &II) –Nyumba hizo zilikwisha uzwa tayari
ii. Nyumba 800-Flats 500 na Villas 300 (PHASE III) ambao umegharimu shilingi bilioni 137.
iii. Mradi wa AZIMIO SATELITE -Kigamboni wenye Nyumba 7160 (Flats &Villas) –Utagharimu shilingi bilioni 871
iv. Mradi wa Dungu Farm-Kigamboni (Flats 568) Utagharimu shilingi bilioni 140
v. Mradi wa MZIZIMA TOWER nyumba ya Ghorofa 32 unaotarajiwa kumalizika Juni 2017, ambao utagharimu shilingi bilioni 233.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni katika hotuba yake ya wizara ya kazi na ajira iliongelea uwekezaji wenye mashaka uliofanywa na Mfuko wa hifadhi ya jamii wa NSSF. Lakini majibu ya waziri aliyekuwa na dhamana yalikuwa ya kisiasa mno badala ya kuangalia ukweli wa kitaalam wa uwekezaji huo kwa kulingana na uwekezaji uliopo na thamani halisi ya ardhi kwa wakati ambao mfuko ulinunua ardhi husika.

### 6.4. MFUKO WA PENSHENI KWA WATUMISHI WA UMMA

**Mheshimiwa Spika**, Kuna mfuko wa pensheni kwa watumishi wa Umma (PSPF) mfuko huu wa hifadhi ulianzishwa kwa sheria Namba 2 ya Mafao ya Hitimisho la Utumishi wa Umma ya mwaka 1999, ikiwa imechukua nafasi ya sheria ya Pensheni Sura 371 ya mwaka 1954, na mfuko ukaanza rasmi shughuli zake Julai 1, 1999.

**Mheshimiwa Spika**,Kwa mujibu wa kumbukumbu za nyaraka zinaonesha kuwa hadi kufikia tarehe 30 Juni 2015 **mfuko unaidai Serikali kiasi cha shilingi bilioni 533.238** zikiwa ni udhamini wa Serikali katika ujenzi wa majengo ya taasisi kadhaa za Serikali, pamoja na mkopo kwa bodi ya mikopo ya elimu ya Juu. **Mbali na fedha hizo Mfuko unaidai Serikali fedha za michango ya wanachama na tozo kwa kipindi cha kuanzia mwezi Agosti 2015** hadi Februari 2016, **kiasi cha shilingi bilioni 305.30.Hiyo ni mbali na deni la** shilingi trillion 6, kutokana na kuwahudumia wastaafu wa zamani ambao hawakuwa katika mfumo wa pensheni.

**Mheshimiwa Spika**, Jambo lingine la kuonesha kuwa hii mifuko kushindwa kusimamiwa, ni kuwa PSPF ilinunua jengo la Quality Plaza(kwa bei ghali tofauti na uhalisia wa jingo) na sasa linaitwa PSPF Plaza kwa shilingi bilioni 36 na

mfuko ukafanya ukarabati kwa gharama ya shilingi bilioni 1.27 lakini mpangaji wake mkuu akawa ni **Yule aliyewauzia jengo hilo,Bwana Yusuph Manji** ,ambaye mpaka anadaiwa shilingi bilioni 13.31 na mkataba wake wa kupanga umeisha lakini bado anaendelea kukaa na amegoma kulipa kodi.

### 6.5. MFUKO WA MAFAO YA KUSTAAFU-GEPF

**Mheshimiwa Spika**, Mfuko huu kama ilivyo mifuko mingine ya hifadhi za jamii, mfuko umejikita katika uwekezaji wa majengo, hisa za makampuni yanayoorodheshwa katika soko la mitaji, amana za Serikali, mikopo serikalini n.k.

**Mheshimiwa Spika**, Takwimu zinaonesha kuwa hadi Juni,2015 uwekezaji katika majengo na ardhi ulifikia kiasi cha shilingi bilioni 25.789. Uwekezaji uliofanywa kwenye ununuzi wa viwanja:

a. Kiwanja na 2401 Kitalu M- kilichopo eneo la Forest – Mbeya chenye ukubwa wa mita za mraba 48,588 kilinunuliwa kwa gharama ya shilingi bilioni 1.6 sawa na kununua mita moja ya mraba kwa shilingi 32,929/-.
b. Kiwanja namba 8 Kitalu E-kilichopo Ilemela Mwanza chenye ukubwa wa mita za mraba 8,191 kilinunuliwa

kwa shilingi bilioni 2 sawa na kununua mita moja ya mraba kwa shilingi 244,170.43/-

c. Kiwanja na. 206 Kitalu H kilichopo Raha Leo Mtwara chenye ukubwa wa mita za mraba 1,428 kilichonunuliwa kwa shilingi milioni 225, sawa na kununua mita ya mraba kwa shilingi 157,563/-
d. Kiwanja Na 207, Kitalu H, mita za mraba 1,424, gharama za kiwanja shilingi 225,000,000/-, gharama kwa mita moja 158,005. Kiwanja kipo Raha Leo Mtwara

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa sheria ya SSRA, Benki Kuu ndio mamlaka ya kuhakikisha mifuko inafanya uwekezaji makini, je kwa uwekezaji huu ambao taarifa ya CAG ilisema kuwa unauweka mfuko katika hali ya kuweza kufilisika na hivyo wanachama kukosa mafao, serikali inatoa majibu gani? Tukumbuke kuwa mfuko huu unaendeshwa na watumishi wengi ambaoni wa kada ya chini na ambao kila mara wamekuwa wakilalamikia mishahara midogo kama walimu na manesi na watumishi wengine wa Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Mifuko ya hifadhi ya jamii ni chombo ambacho kama kikisimamiwa vyema katika uwekezaji wake na pia kuwepo kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za wanachama ingeweza kutekeleza miradi mingi

mikubwa kama vile miradi ya umeme na mradi wa reli badala ya kutafuta mwekezaji kutoka nje ya nchi. Miradi hii ni dhahiri ingeweza kurejesha gharama za uwekezaji haraka, badala yake uwekezaji unafanyika mkubwa unafanyika kwenye miradi ya majengo miradi ambayo urejeshwaji wa gharama za uwekezaji sio wa haraka.

**Mheshimiwa Spika,Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni** inaitaka serikali kumuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za serikali (CAG) kufanya ukaguzi maalum kwenye mifuko yote ya hifadhi ya jamii na kuangalia kama mikataba na uwekezaji ambao ulifanywa na mashirika haya una tija kwa mashirika yenyewe,Wanachama wa mifuko hiyo na taifa kwa ujumla .

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kupitia kwa mdhibiti wa mifuko ya hifadhi ya jamii (SSRA) itoe tathmini ***square meter*** moja ya ardhi yalipojengwa majengo yaliyojengwa na mifuko katika maeneo mbalimbali hapa nchini ilinunuliwa kwa shilingi ngapi?

### 6.6. FAO LA KUJITOA (WITHDRAWAL BENEFIT)

**Mheshimiwa Spika,**katika Bunge la 10, mwaka 2012 kulitokea mtafaruku mkubwa sana kwa wafanyakazi hasa

wale wanafanyakazi kwenye migodi, kutokana na ukweli kwamba masharti yaliyowekwa kwa wanaotakiwa kunufaika na pensheni (fao la uzeeni) ni lazima uwe umechangia mfuko kwa kipindi cha miezi 180 au miaka 16 na pia awe ametimiza umri wa miaka 55.

**Mheshimiwa Spika,** Mbunge wa Kisarawe wakati alipewa kazi na Bunge kukutana na wadau na kutoa mapendekezo ni kwa jinsi gani kanuni na sharia zitaweza kurekebishwa ili kuondoa usumbufu kwa fao hilo la kujitoa, na wadau walitoa ushauri na maoni. Na kwa bahati mbaya tarehe 23 mei, 2016, Msemaji wa PPF alitangaza kuwa fao hilo la kujitoa limefutwa.

**Mheshimiwa Spika,** mazingira yanaonesha kuwa wastani miaka ya kufanyakazi katika sekta ya migodi ni miaka 5, na wastani wa umri wa watumishi katika sekta hiyo ni miaka 35. Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba watumishi wengi ambao ni wa mkataba na wanachangia lakini hawana uwezo wa kuchangia katika mifuko kwa kipindi cha miaka 15 na pia wengine inawalazimu wakae miaka zaidi ya 15 au 20 ndipo wafikishe umri wa miaka 55.

**Mheshimiwa Spika,** hoja ni kuwa fedha hizo hata kama ni milioni kadhaa ziko katika mifuko ya hifadhi, kwa kuwa vigezo havikutimia hadi unafikisha miaka hiyo ya kisheria bado fedha utakazolipwa ni zile zile, na kutokana na

mazingira ya kiuchumi ni dhahiri thamani ya shilingi kwa dolla ikashuka sana. Kambi Rasmi ya Upinzani inamtaka waziri wa Fedha kuliangalia suala hili vizuri ili kuepusha madhara makubwa yanayoweza kuwapa wahusika wakuu ambao ni watumishi wa mikataba na migodini.

## 7. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** kama ambavyo tumejadili kuhusu umuhimu wa wizara ya fedha katika mustakabali mzima wa uchumi wanchi yetu na pia ni wizara hiyo hiyo inayohusika na masuala ya yote ya kodi za bidhaa na huduma.

**Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa wizara hii inachangamoto nyingi na kubwa katika kutekeleza majukumu yake, lakini hilo haliondoi ukweli kwamba ni jukumu lake la msingi ya kuhakikisha watanzania wanaishi katika nchi yao wakiwa na utulivu wa akili **"peace of mind".** Kwa maana kuwa watanzania wanaweza kuishi katika kiwango kinachokubalika na kuweza kutekeleza majukumu ya msingi ya kifamilia, kwani uchumi wa mtanzania kukua ni lazima uakisi katika maisha binafsi ya watanzania.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

………………………………

**David Ernest Silinde (Mb)**

**Naibu Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**

**Wizara ya Fedha na Mipango**

**1st Juni, 2016**